HISTORIA YA PAROKIA

Utangulizi.
Parokia ya Mwenyeheri Anwarite, Makuburi ilianza kama Kigango chini ya Parokia ya Moyo Mtakatifu wa Yesu, Manzese. Msimamizi na Mwombezi wetu ni Mwenyeheri Sista Maria Clementina Anwarite. Siku ya kumbukumbu yake ni tarehe 1 Desemba kila mwaka. Mapadre wa wakati huo walikuwa chini ya Shirika la Wamisionari wa Afrika (White Fathers).

Uanzilishi wa Kigango.
Mwaka 1986, jitihada za kutafuta kiwanja cha kujenga Kanisa la Kigango zilifanyika chini ya Paroko wa Parokia ya Manzese, Padre Gerald Chebanon. Baada ya yeye kuondoka ziliendelezwa na Padre Jean-Francois Galtier, Maparoko wasaidizi Padre George Smith na Padre Raymund Echeveria, wakishirikiana na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Walei Parokia ya Manzese ndugu Gislar K. Zullu. Katika jitihada hizo tunamshukuru Mungu, kwani Halmashauri ya Jiji ilitupa kiwanja bila malipo yoyote, na baadaye tuliongeza eneo la Kanisa kwa kununua nyumba za majirani.

Uzinduzi wa Kigango.
Tarehe 18/08/1988, Kigango cha Makuburi kilizinduliwa kwa ibada ya misa Takatifu iliyoadhimishwa na Paroko wa Parokia ya Manzese Padre Jean-Francois Galtier. Kigango cha Makuburi kiliendelea kuwa chini ya Parokia ya Manzese kwa miaka 9 (1988-1997).

Parokia Teule.
Tarehe 16/05/1997, Askofu Mkuu wa Jimbo kuu la Dar es Salaam, Baba Mwadhama Polycarp Kardinal Pengo alikiteua Kigango cha Mwenyeheri Anwarite, Makuburi kuwa Parokia Teule ya Makuburi.

Uzinduzi wa Parokia.
Tarehe 02/08/1997, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo alizindua rasmi Parokia ya Mwenyeheri Anwarite Makuburi katika adhimisho la Misa Takatifu, na alimsimika Padre Gerald Derksen kuwa Paroko, na Paroko msaidizi alikuwa Padre Brian Mkude.

Upanuzi wa Kanisa.
Jiwe la msingi la Kanisa liliwekwa rasmi na aliyekuwa Balozi wa Baba Mtakatifu nchini Mhashamu Baba Askofu Mkuu Francisco Javier Lozzana katika adhimisho la misa takatifu tarehe 01/05/1998. Ujenzi ulikamilika na jiwe la ufunguzi wa Kanisa liliwekwa na Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo tarehe 12/12/1998.

Parokia ilipo (Jiografia):-
- Kata ya Makuburi, wilaya ya Ubungo katika mkoa wa Dar es Salaam.
- Katika Dekania ya Ubungo.
- Inapakana na shule za msingi Mabibo/Makuburi na Export Processing Zone Authority (EPZA).
- Parokia yetu inapakana na:-
  Parokia ya Msewe upande wa Kaskazini, Parokia ya Kibangu upande wa Kaskazini Magharibi, Parokia ya Makoka upande wa Magharibi, Parokia ya Kimanga upande

wa Kusini Magharibi, Parokia ya Manzese upande wa Mashariki, Parokia ya Luhanga upande wa Kusini Mashariki, Parokia ya Tabata Kisiwani upande wa Kusini.

Maparoko waliohudumu kuanzia mwaka 1997 hadi sasa 2018.

Padre Gerald Derksen	1997 - 2006
Padre Nicolaus Pesambili Masamba	2006 - 2010
Padre Faustine Mlelwa	2010 - 2012
Padre Jovin Bakekera	2012 - hadi sasa 2018

Maparoko wasaidizi waliohudumu kuanzia mwaka 1997 hadi sasa 2018.

Padre Brian Mkude	1997 - 2000
Padre Ireneus Mbahurila	1999 - 2003
Padre George Sayi	2000 - 2006
Padre Sixtus Kimaro	2003 - 2003
Padre Romuald Mukandara	2004 - 2005
Padre Nicolaus Pessambili Masamba	2006 - 2006
Padre Gallen Mvungi	2007 - 2011
Padre James Mweyunge	2009 - 2010
Padre Christian Likoko	2010 - 2011
Padre Joseph Mapunda	2011 - 2015
Padre Joseph Kazikunema	2015 - 2016
Padre Paschal Kamugisha	2016 - hadi sasa 2018

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Kigango cha Makuburi 1988-1997

Mwenyekiti	Ndugu Gislar K. Zullu
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Stanslaus S. Kazimoto (Marehemu)
Katibu	Ndugu Peter Felix
Katibu Msaidizi	Katekista John Mwalyenga

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 1998 - 2001

Mwenyekiti	Ndugu Gislar K. Zullu
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Adrian Mpande (Marehemu)
Katibu	Ndugu Monica Changamike
Katibu Msaidizi	Ndugu Casmir Massawe
Mhazini	Ndugu Roman Kavishe (Marehemu)

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 2001 - 2003

Mwenyekiti	Ndugu Bruno Hinju
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Humphrey Lyimo
Katibu	Ndugu Monica Changamike
Katibu Msaidizi	Ndugu Casmir Massawe
Mhazini	Ndugu Boniface Lesso

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 2003 - 2006

Mwenyekiti	Ndugu January Kisanko (Marehemu) / Ndugu Lucas Mushi
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Edwin Mikongoti / Ndugu Herman Sichalwe (Marehemu)
Katibu	Ndugu Monica Changamike / Ndugu Buberwa
Katibu Msaidizi	Ndugu Lucian Kikoti
Mhazini	Ndugu Boniface Lesso

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 2006 - 2009

Mwenyekiti	Ndugu Fortunatus Nzota (Marehemu)
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Peter Felix
Katibu	Ndugu Wilhelmina Malima
Katibu Msaidizi	Ndugu Agino Safari
Mhazini	Ndugu Bonitas Mwaleni

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 2006 - 2009

Mwenyekiti	Ndugu Fortunatus Nzota (Marehemu)
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Peter Felix
Katibu	Ndugu Wilhelmina Malima
Katibu Msaidizi	Ndugu Agino Safari
Mhazini	Ndugu Bonitas Mwaleni

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 2010 - 2013

Mwenyekiti	Ndugu Jackson S. Mtoka
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Prudence Mgobe
Katibu	Ndugu John C. Mgaka
Katibu Msaidizi	Ndugu Arodia Ndena
Mhazini	Ndugu Vedastus Namwata

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 2013 - 2016

Mwenyekiti	Ndugu Jackson S. Mtoka
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Herman Sichalwe (Marehemu) / Ndugu Mary J. Kimaro

Katibu	Ndugu John C. Mgaka
Katibu Msaidizi	Ndugu Felista Sengerere
Mhazini	Ndugu Vedastus Namwata

Kamati tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia ya Makuburi 2016 - mpaka sasa 2018

Mwenyekiti	Ndugu Mary J. Kimaro
Makamu Mwenyekiti	Ndugu Johanes Rwezaula
Katibu	Ndugu Bernard Mukasa
Katibu Msaidizi	Ndugu Felista Sengerere
Mhazini	Ndugu Vedastus Namwata

Watawa wa kike.
Toka mwaka 1997 mpaka sasa Parokia yetu inahudumiwa na Masista wa Shirika la Bikira Maria Malkia wa Mitume wa Jimbo la Mbeya.

Vigango.
Kwa sasa Parokia haina Kigango, lakini iliwahi kuwa na vigango 7 navyo ni:-

1. Kigango cha Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni - Ubungo Kibangu, tayari ni Parokia tangu mwaka 2000.
2. Kigango cha Mt. Theresia wa Mtoto Yesu - Nzasa, kilihamishiwa Parokia ya Kibangu, tayari ni Parokia tangu mwaka 2015.
3. Kigango cha Mt. Gaudensi - Makoka, tayari ni Parokia tangu mwaka 2010.
4. Kigango cha Bonyokwa, kwa sasa ni Kigango cha Parokia ya Mt. Gaudens, Makoka.
5. Kigango cha Mt. Monica - Kilungule, kilihamishiwa Parokia ya Kibangu, tayari ni Parokia tangu mwaka 2011.
6. Kigango cha Mt. Yohana Mbatizaji - Luhanga, tayari ni Parokia tangu mwaka 2005.
7. Kigango cha Mt. Padre Pio - Tabata Kisiwani, tayari ni Parokia tangu 2016.

Muundo wa utawala wa Parokia.



Muundo wa Parokia.

- Parokia ina jumla ya kanda 10 nazo ni:-

  - Mt. Yohane Paulo XIII - Papa, Relini.
  - Mt. Anyesi, Mandela.
  - Mt. Ritha wa Kashia, Ubungo Kisiwani.
  - Mt. Yohane Mtume na Mwinjili, Ubungo Maziwa.
  - Mt. Yohane Paulo II - Papa, Makuburi.
  - Mt. Gregory Mkuu - Papa, Gereji.
  - Mt. Katarina wa Siena, Mikongeni.
  - Mt. Theresa wa Kalkutta, Jeshini.
  - Mt. Mathayo Mtume na Mwinjili, Redio.
  - Mt. Leo Mkuu - Papa, Maji.

- Parokia ina jumla ya Jumuiya ndogondo za Kikristo 73.

- Parokia ina jumla ya waamini 6,100, kulingana na sensa ya mwaka 2017.

Wanawake	1,765
Wanaume	2,014
Watoto	2,771
Jumla	**6,100**

- Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume vipo 11.

  - Moyo Mtakatifu wa Yesu.
  - Shirika la Utoto Mtakatifu wa Yesu.
  - Legio Maria.
  - Vincent De Paul
  - CPT (Christian Proffesionals of Tanzania)
  - WAWATA (Wanawake Katoliki)
  - UWAKA (Wanaume Katoliki)
  - VIWAWA (Vijana Katoliki)
  - SHIKWAKA (Shirikisho la Kwaya: - Mt. Kizito, Mwenyeheri Anwarite na Mt. Cecilia)
  - Kolping
  - Karismatiki Katoliki

Ratiba za Misa.

Dominika kuna Ibada za Misa 4:-

- Misa ya 1 inaanza saa 12:00 asubuhi.
- Misa ya 2 inaanza saa 1:30 asubuhi.
- Misa ya 3 inaanza saa 3:20 asubuhi.
- Misa ya 4 inaanza saa 5:00 asubuhi.

Misa za kila siku katika juma:-

- Jumatatu - Ijumaa, misa zinaanza saa 12:30-1:00 asubuhi.

- Jumamosi misa inaanza saa 1:00-1:30 asubuhi.

- Alhamisi misa inaanza saa 10:30-11:00 Jioni.

Kuabudu Ekaristi Takatifu.
- Ni kila Alhamisi, inaanza saa 11:00-12:00 jioni.

Ratiba ya Sakramenti ya kitubio.

- Jumatatu-Ijumaa, kila baada ya Misa ya juma.
- Jumamosi, baada ya Misa ya ndoa.

Sakramenti nyingine.

Zinatolewa kama kawaida kulingana na uhitaji wa waamini.

Saa za Ofisi.

- Jumatatu-Ijumaa kuanzia saa 2:00-6:30 mchana
  saa 9:00-12:00 jioni.
- Jumamosi kuanzia saa 2:00-6:00 mchana.
- Jumatano ofisi zinafungwa.

Huduma za kiroho.

- Waamini wanashiriki Misa Takatifu katika Jumuiya ndogondogo za Kikristo na kanda.
- Waamini wanapata mafundisho ya Sakramenti mbalimbali.
- Waamini wanashiriki maisha ya sala katika Jumuiya ndogondogo za Kikristo.
- Waamini wanashiriki Misa Takatifu siku za juma na Dominika.
- Waamini wanashiriki Ibada mbalimbali hapa Parokiani (Kuabudu Ekaristi Takatifu, kusali Rozari, n.k.)
- Waamini wanashiriki semina na mafungo mbalimbali.
- Waamini wamejiunga kwenye Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume ili kukuza Imani.
- Wanaparokia wanashiriki Hija mbalimbali.
- Kutembelea wagonjwa na wazee wanaoshindwa kufika Parokiani.
- Timu ya Uinjilishaji inatembelea jumuiya na kanda zote ili kukuza imani.

Huduma za kimwili.

- CHEMA (Chuo cha Elimu ya Maisha): Shule hii inatoa elimu ya msingi kwa mpango wa MEMKWA kwa watoto/vijana walioshindwa kujiunga na elimu ya msingi wakiwa na umri mdogo na ambao wanaishi katika mazingira magumu (wahitaji). Inapokea vijana wa jinsia zote, madhehebu yote na dini zote.
- Kupitia Parokia, wanaparokia waliohitaji bima ya afya wanazo kadi za bima ya afya kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).
- VICOBA kwa wakina mama.

Tunda la Kanisa.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia Padre Denis Ananias Wigira, ambaye ni mzawa wa Parokia hii.

Changamoto.

- Eneo dogo la Parokia yetu, hivyo tuko kwenye mkakati wa kununua nyumba za majirani ili kuongeza eneo.
- Wanaparokia wengi ni wapangaji, hivyo ni ngumu kuwa na idadi kamili ya wanaparokia na kila mara tunafanya uchaguzi mdogo kuziba nafasi za viongozi wanapohama.

Hitimisho.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote aliyotujalia mpaka tumefika hapa tulipo na tunamuomba azidi kutujalia ili tusonge mbele zaidi kulijenga Kanisa lake. Mwenyeheri Anwarite msimamizi na mwombezi wetu utuombee.